

**HOTUBA YA MHE. ABBAS KANDORO, MKUU WA MKOA WA
DAR ES SALAAM WAKATI AKIFUNGUA KIKAO CHA KAMATI YA
USHAURI YA MKOA KILICHOFANYIKA TAREHE 20 NOVEMBA,
2008 KATIKA UKUMBI WA ARNAUTOGLO**

Wajumbe wa Kamati ya Ushauri ya Mkoa,

Katibu wa CCM wa Mkoa,

Waalikwa wote,

Mabibi na Mabwana.

Ninapenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha katika kikao cha kawaida cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Dar es Salaam. Madhumuni ya Kikao hiki ni kutoa ushauri katika mambo mbali mbali kuhusu masuala ya maendeleo ya jamii, kiuchumi na uendeshaji utawala. Hivyo, katika kikao hiki kila mmoja awe makini kuibua mbinu zitakazotuwezesha kufikia ufanisi unaotakiwa. Ninatarajia mtajikita zaidi katika maeneo yafuatayo:-

- i) Utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika ngazi ya Halmashauri uzingatie mtazamo wa Serikali wa kupeleka madaraka na fedha nyingi katika ngazi za Serikali za Mitaa. Lengo kuu ni kuwezesha mamlaka hizo kuzitumia fedha zilizoidhinishwa kwa mambo muhimu yaliyopangwa na kwa utekelezaji wenye ufanisi tukitarajia kuona 'value for money'.

- ii) Usimamizi wa utekelezaji wa mambo ambayo yameamuliwa uwe thabiti ukitekelezwa kwa ushirikiano kati ya viongozi na wananchi na wadau wengine wa maendeleo. Nachelea kusema kuwa jitihada zetu za kusimamia bado hazitoshelezi na ndiyo maana tunaonekana kushindwa kuyaenzi mambo ambayo kwa hakika tulikwishajipatia ufanisi. Sasa machinga wapo mtaani kama kawaida, uchafu unazidi kuonekana kuzagaa, omba omba wapo, vurugu katika barabara bado ni kubwa kwa kuwa watu hawaheshimu sheria zilizopo nasi tunashindwa kusimamia utekelezaji wa sheria hizo. Si budi tutafakari namna ya kufanikiwa.
- iii) Tutafakari kuhusu matatizo ya miundombinu ambayo ni finyu, michache, mibovu na ambayo haikidhi mahitaji ya Mkoa huu. Fedha zinazotengwa kwa ajili ya miundo mbinu hususan ya barabara zitumike vizuri kuboresha miundombinu na mazingira ya maisha ya wananchi.
- iv) Wanafunzi wapatao 38,925 wanatarajiwa kufaulu mtihani wa darasa la saba kati ya wanafunzi 64,877 waliofanya mtihani. Kwa mujibu wa agizo la Serikali tuliloletewa ni kwamba Wanafunzi wote watakaofaulu tuhakikishe wamejiunga na kidato cha kwanza. Miundombinu ya elimu bado haitoshelezi idadi hiyo. Tutafakari.

Tunayashughulikia matatizo ya Wanafunzi, nafurahi kusema madai ya Walimu nayo tunaendelea kuyatazama.

Halmashauri zetu zimekwisha pokea kiasi chote tulichoomba (SHS.1,828,000,000/=) kulipia madai ya Walimu. Nawashauri Walimu watakao kuwa na madai waende kwa Mwajiri. Aidha, Halmashauri zisitoe maamuzi yanayoweza kuongeza madai ya Walimu kama uhamisho: Wafanye hivyo.

- v) Kufanya kazi kama timu moja ni nyenzo ya ushindi. Kila mmoja atekeleze wajibu wake na ufanisi atakaopata uwe daraja la mwingine kufanikiwa katika eneo lake. Tusitegeane na kufikiria kuwa hii ni kazi ya fulani na hii ni ya kwangu bali tushauriane, tuelekezane, na tusaidiane huku tukiongozwa na sheria, taratibu, kanuni, sera na miongozo mbali mbali iliyopo.
- vi) Mawasiliano ni sehemu muhimu ya kuyafanya mambo mbali mbali kufanyika. Ninawashauri watendaji wote katika Mkoa kulipa umuhimu suala la mawasiliano. Kila ngazi katika uongozi wa nchi inapenda kujua mambo yanavyoendelea kutekelezwa na kwa ufanisi gani. Hivyo, tusinyimane taarifa, tusizicheleweshe zinapohitajika na tutoe taarifa zenye usahihi zinazoeleza hali halisi.

Haya ni mambo machache ambayo nimeona ni vema niyatilie mkazo na yawe kiongozi cha kikao cha kamati hii.

Ninarudia tena kuwakaribisha katika kikao hiki na muwe wazi katika kuchangia utatuzi wa changamoto zinazotukabili. Baada ya kusema hayo ninatamka rasmi kuwa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa kimefunguliwa.

Asanteni.